# Kupiga Simu 911 – Simu za Dharura

**(Huduma za ukalimani zinapatikana)**

Dharura ni wakati wowote ambapo Maisha, usalama na mali ya mtu fulani inapokuwa inakabiliwa na hatari ya *moja kwa moja* au kuna uhalifu unaendelea. Hapa chini kuna mwongozo wa kile cha kukitarajia na vidokezo vya kukusaidia.

## Kile cha Kukitarajia

- Mfumo unakuelekeza kwenye kituo cha waraka wa usalama wa umma kilicho karibu nawe.
- Nani, Nini, Wapi: Huelezea kwa nini unapiga simu na kueleza kama hali hiyo bado inaendelea au la.
- Maswali ya mwendeshaji yatakuongoza.
- Taja eneo/anwani kamili ambapo msaada unahitajika, ikiwemo taarifa kuhusu namba ya ghorofa, namba ya chumba, eneo ndani ya jengo.
- Taja jina lako, eneo lako la sasa nanamba ya simu.
- Usikate simu. USIKATE simu hadi pale mwendeshaji atakaporuhusu simu yako. Hali hubadilika kila wakati na taarifa mpya inaweza kuhitajika.

## Vidokezo

- Endelea kutulia – vuta pumzi.
- Jibu maswali yote na fuata maagizo kama ulivyoelekezwa.
- Unapomuelezea mtu jumuisha taarifa kuhusu urefu, unene, mavazi na sifa za kipekee (kovu, tattoo, nywele za uso).
- Unapoelezea gari jumuisha aina ya gari, rangi, muundo (milongo 2, milango 4), sifa bainishi, namba ya gari (namba – kamili au kiasi, rangi ya bampa la namba ya gari, jimbo).
- Mahali ambako gari au mtu (kama anatembea kwa miguu) anaelekea.
- Watumiaji wa simu ya mkononi: Anwani yako haionekani kwa mwendeshaji; simu ya mkononi itaorodhesha latitudo na longitudo.

# Simu Zisizo za Dharura – 242-COPS (2677)

**(Huduma za ukalimani zinapatikana)**

Hali isiyo ya dharura ni pale ambapo Maisha, usalama au mali ya mtu fulani haipo kwenye hatari ya moja kwa moja, lakini majibu ya polisi yanahitajika.

## Aina ya hali zisizo za dharura

- Wizi Katika Makazi – kwa kuchelewa au mhalifu kutokuwepo katika tukio
- Wizi katika Biashara – kwa kuchelewa kwa muda au hakuna mkosaji kwenye eneo la tukioSherehe kubwa
- Shughuli Inayotiliwa Shaka

## Kitengo cha Kuripoti kwa Simu

- Wizi wa Magari
- Wizi wa Kuvunja Magari
- Wizi wa Utambulisho
- Kuharibu Mali
- Wivu
- Mali Iliyopotea

# Nyenzo za Ziada

- Kuripoti mtandaoni (Kiingereza pekee): https://www.cabq.gov/police/file-a-police-report-online
- Programu ya APD: Tafuta Atlas One kwenye Google Play au App Store
- Ripoti za Vituo Vidogo: Ripoti za Ajali; Ripoti za Makosa bila taarifa za mtuhumiwa
- Ulemavu wa Kusikia au Kuzungumza: Kituo cha waraka za usalama wa umma kina TTY/TDD ili kuwezesha mawasiliano na kifaa chako.
- Ujuzi Mdogo wa Kiingereza: Waendeshaji wanaweza kupata huduma za ukalimani kwa njia ya simu katika mamia ya lugha.